## Maswali

1. Mungu aliahidi Wayahudi nini?
2. Nani alitengeneza sheria eti Wayahudi warudi Israeli?
3. Koreshi aliwapa Wayahudi nini waende nayo Yerusalemu?
4. Wayahudi walijenga nini Yerusalemu?
5. Kuhani alikuwa nani aliyeenda kuishi Yerusalemu?
6. Ezra alifundisha Wayahudi nini?
7. Kazi ya Nehemia ilikuwa gani?
8. Mbona Nehemia aliuliza mfalme ili aende Yerusalemu?
9. Nehemia na Wayahudi walijenga nini?
10. Wayahudi walifanya nini maadui walipojaribu kuwasimamisha wasijenge?

## Majibu

1. Baada ya miaka 70 wangeenda kuishi kwa nchi ya Israeli tena.
2. Mfalme Koreshi aliweka sheria kwamba Wayahudi wanaweza kurudi Israeli.
3. Koreshi aliwapa vikombe na bakuli za dhahabu na fedha wapeleke kwa Hekalu.
4. Wayahudi walijenga Hekalu Yerusalemu.
5. Ezra ni kuhani aliyeenda Yerusalemu.
6. Kuheshimu sheria za Mungu. Kujitenga na wanaoabudu sanamu.
7. Nehemia alikuwa mnyweshaji wa mfalme.
8. Nehemia aliuliza aende Yerusalemu kwa sababu kuta zilikuwa zimeanguka.
9. Nehemia na Wayahudi walijenga tena kuta za Yerusalemu.
10. Waliweka walinzi kuangalia maadui. Walibeba silaha wakati wa kujenga.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 2 Mwaka wa 2

# 85 Ezra na Nehemia

### Kwa Biblia

Ezra mlango ya 1 & 3 na mlango wa 7:1-10
Nehemia mlango wa 1 & 2

### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu hujibu maombi. Mungu hufurahi ikiwa tunamfanyia kazi.

### Somo

Mungu alifanya ahadi na watu wake, Wayahudi. Mungu alifanya hii ahadi kabla Wayahudi hawajachukuliwa mateka huko Babeli. Mungu aliwaahidi kwamba baada ya miaka 70, watarudi kwa nchi yao. Mungu aliwambia Wayahudi kwamba watakuwa wafungwa Babeli kwa miaka 70. Lakini aliwaahidi kwamba baada ya miaka 70 watarudi kwa nchi ya Israeli. Watajenga Yerusalemu na Hekalu ya Mungu.

Mfalme Nebukadreza alishinda na kuchukua Yerusalemu. Alichukua Wayahudi kama mateka mpaka Babeli. Miaka 70 baadaye Mfalme Koreshi alipiga na kuchukua Babeli. Mfalme Koreshi alijua kwamba Mungu ni Mungu wa kweli. Koreshi alitengeneza sheria kwamba Wayahudi wanaweza kurudi na kuishi kwa nchi yao na wajenge Hekalu tena. Kila kitu kilikuwa vile Mungu alikuwa ameahidi.

Zaidi ya Wayahudi 42,000 walitaka kwenda kuishi kwa nchi ya Israeli. Wayahudi wengine hawakutaka kurudi huko. Walitaka kuishi Babeli. Hawa Wayahudi walipeana dhahabu na fedha za kuenda kusaidia kujenga Hekalu tena. Mfalme Koreshi alirudisha vikombe vya dhahabu na fedha vyenye Nebukadreza alichukua kutoka kwa Hekalu.

Zerubabeli na Yoshua waliongoza Wayahudi 42,000 kwenda Israeli. Walichukua dhahabu yote na fedha wakapeleka kwa Hekalu.

Wayahudi wengi walikuwa wamezaliwa Babeli. Walikuwa hawajaona nchi waliyopewa na Mungu. Kila mtu alifurahi kwenda kuishi kwa nchi ya Israeli. Wayahudi walifurahi kwa sababu Mungu alikuwa ametimiza ahadi yake. Walifurahi kuwa kwa nchi ya Israeli. Wayahudi wengi walienda kuishi Yerusalemu. Wayahudi walianza kujenga Hekalu tena. Maadui wao walijaribu kuzuia wasijenge. Kwa muda ujenzi wa Hekalu ulisimama. Lakini mwishowe Hekalu ilimalizika. Wayahudi walikuwa na sherehe kubwa. Waliweka Hekalu wakfu na wakaabudu Mungu kule.

Ezra alikuwa kuhani mwaminifu. Aliishi Babeli. Ilikuwa kama miaka 60 tangu Wayahudi warudi Yerusalemu na kujenga Hekalu tena. Ezra aliamua kwenda na aabudu Mungu kwa Hekalu Yerusalemu. Aliuliza Mfalme ili aende kuishi kwa nchi ya Israeli. Mfalme alimpa ruhusa ya kuenda kuishi kwa nchi ya Israeli. Na alimwambia kwamba anaweza kwenda na Wayahudi wanaotaka kwenda kuishi Israeli.

Mfalme alipea Ezra dhahabu na fedha akienda ili apelike kwa Hekalu. Alimtawaza Ezra kuwa liwali wa Yerusalemu. Ezra alienda Yerusalemu kufundisha watu sheria za Mungu. Alienda na Wayahudi wengi waliotaka kwenda kuishi kwa nchi ya Israeli. Ezra na Wayahudi waliwasili Yerusamu salama. Walishukuru Mungu na kumwabudu katika Hekalu.

Wayahudi wengi Yerusalemu walikuwa wameoa wanawake wageni. Walikuwa wameasi Mungu. Ezra alikasirika sana. Wayahudi walikuwa wamekuwa wafungwa Babeli kwa miaka 70. Walichukuliwa huko mateka kwa sababu waliasi Mungu. Sasa walikuwa wanaasi Mungu tena. Ezra aliomba Mungu awasamehe. Ezra alifundisha Wayahudi sheria za Mungu. Wayahudi waliahidi kutii Mungu.

Ezra alifanya kazi kubwa sana Yerusalemu. Alifundisha Wayahudi kuabudu Mungu. Aliwafundisha kutengana na watu wanaoabudu sanamu.

Kuta za Yerusalemu zilikuwa bado zimebomoka. Hazikuwa zimejengwa. Mawe yalikuwa yamelundikana na kufunga barabara. Lango za Yerusalemu zilikuwa zimechomwa. Wayahudi walikuwa na maadui wengi. Mji wa Yerusalemu haukuwa umekingwa. Wayahudi walikuwa kwa shida.

Nehemia alikuwa ni mnyweshaji wa Mfalme wa Babeli. Alikuwa mtu wa maana sana. Nehemia alikuwa akimwagia Mfalme divai kwa kikombe. Ndiye alikuwa akionja divai kama kuna sumu.

Kuna Wayahudi waliokuja Babeli. Waliambia Nehemia kwamba Wayahudi walikuwa kwa shida. Walimwambia kwamba kuta za Yerusalemu zilikuwa zimebomoka. Nehemia aliudhika sana kwa ajili ya habari hiyo. Mfalme aliuliza Nehemia mbona hakukuwa na furaha. Nehemia aliambia Mfalme kwamba watu wake, Wayahudi walikuwa na shida. Kuta za Yerusalemu zilikuwa zimebomoka. Nehemia aliomba Mungu kwanza, halafu akaenda kuuliza Mfalme ampe ruhusa aende Yerusalemu ili ajenge kuta tena. Mfalme aliruhusu Nehemia aende Yerusalemu. Alipea Nehemia pesa za kutumia kujenga kuta.

Nehemia alienda Yerusalemu. Alizunguka kuta zote kwa punda ili angalie vile ilikuwa imebomoka. Alizungumza na wasimamizi wa Wayahudi. Walikubaliana kujenga kuta tena, Watu wengi wa Yerusalemu walisaidia kufanya hiyo kazi.



Walifanya kazi ya kujenga kwa vikundi vidogo vidogo. Kila mtu alisaidia. Walifanya kazi pamoja, waume kwa wake. Wengine walifanya kidogo na wengine nyingi. Lakini walisaidiana wote. Walikuwa na imani kwamba Mungu atasaidia.

Wayahudi walikuwa na maadui wengi. Maadui walijaribu kuzuia kazi. Lakini waliendelea kujenga. Waliweka walinzi ili wachunge maadui. Wayahudi walijenga wakiwa na silaha kwa mkono moja. Mungu aliwasaidia. Walimaliza kujenga kuta za Yerusalemu kwa siku 52.

Nehemia alikuwa msimamizi mkuu. Alikuwa akiomba Mungu wakati kulikuwa na ugumu. Nehemia aliamini Mungu wakati wote. Hakuogopa maadui wake. Alijua kwamba Mungu angesaidia. Nehemia alisaidia Wayahudi kujenga kuta za Yerusalemu tena. Kwa hivyo Wayahudi walikaa salama Yerusalemu.